SHINYANGA REGION CO-OPERATIVE UNION (1984) LTD.
BULUBA SECONDARY SCHOOL

S.L.P. 173, SHINYANGA Tel. No 028 – 2763380 Mob. 0764 478683/0683501913
Email: bulubass@yahoo.com

Tarehe 02 FEBRUARY, 2018

Jina la Mwanafunzi: …….
Kidato cha TANO

YAH: **MAAGIZO MUHIMU KWA WANAFUNZI WOTE WA HOSTEL WANAOINGIA KIDATO CHA TANO**

1. **TAREHE YA KUANZA MASOMO**:

   Masomo yataanza rasmi tarehe 02 July mwaka 2018. Wanafunzi wote wanatakiwa kufika shuleni saa 1 na dakika 30 asubuhi.

2. **NGUO ZA KUANZIA MASOMO:**

   Kabla ya kupata sare rasmi za Shule, wanafunzi wote wavae sare za Shule za Sekondari walikomalizia kidato cha 4 mwaka jana. Wanafunzi wote watavaa viatu vyeusi vya ngozi, ambavyo vitakuwa nusu mviringo kwa upande wa mbele. Viatu vya mstatiri (square) havitakiwi. Visigino vya viatu visiwe virefu (Raizoni). Wasichana watavaa soksi fupi nyeupe.

3. **SARE RASMI ZA SHULE:**

   Sare rasmi za shule zinauzwa shuleni. Sare za shule zifuatazo zitanunuliwa hapa hapa shuleni. Ili kupata sare, mwanafunzi awasiliane na Makamu Mkuu wa Shule Mwalimu Makoye Nzala.

WAVULANA			**WASICHANA**		
AINA YA SARE	**IDADI**	**BEI YAKE**	**AINA YA SARE**	**IDADI**	**BEI YAKE**
T – shirt nyekundu na “Light Blue”	02	20,000/=	T – shirt nyekundu na “Light Blue”	02	20,000/=
Sweta la Bluu	01	16,000/=	Sweta la Bluu	01	16,000/=
Shati 2 nyeupe za mikono mirefu	02	26,000/=	Shati 2 nyeupe za mikono mirefu	02	25,000/=
Suruali 2 za Bluu (Dark blue)	02	36,000/=	Sketi za Bluu (Dark blue)	02	24,000/=
Suruali 2 nyeusi	02	36,000/=	Sketi 2 nyeusi na kizibao kimoja	02	30,000/=
Tai	01	5,000/=	Tai	Hakuna	-
Shuka za pink (za pamba)	03	30,000/=	Shuka Light Blue (za pamba)	03	30,000/=
Godoro na mto TAN FOAM 2½ x 4 x 6	01	55,000/=	Godoro na mto TAN FOAM 2½ x 4 x 6	01	55,000/=
Neti ya mbu	01	10,000/=	Neti ya mbu	01	10,000/=
Mkanda wa suruali	01	6,000/=	Mkanda Hakuna	01	-
JUMLA		240,000/=	**JUMLA**		210,000/=

Sare zote za shule zitanunuliwa shuleni. Usinunue sare za shule nje ya shule yetu. Huu ndiyo utaratibu wetu. Fedha za sare zilipwe kwenye akaunti ya Shule ya Sare.

3:1 **HIJABU:**

Wanafunzi Wasichana Waislamu wanaotaka kuvaa HIJABU watalipa Tshs. 90,000/= (tisini elfu) na watashonewa jozi mbili za Hijabu. Lipa fedha za HIJABU kwa **Mhasibu wa Shule.**

Fedha zote za sare zilipwe kwenye Akaunti ya Shule ya sare, Akaunti namba **024101001930** NBC Shinyanga. Baada ya kulipa leta "Bank pay in slip" kwa Mhasibu wa shule.

4. **ADA YA MASOMO NA HOSTEL:**

Ada za masomo na Hosteli zitakuwa kama ifuatavyo:

MUHULA WA KWANZA			MUHULA WA PILI	
NA.	**MAELEZO**	**MALIPO YAKE**	**MAELEZO**	**MALIPO YAKE**
1.	Ada ya Masomo	350,000/=	Ada ya Masomo	350,000/=
2.	Ada ya Bweni	130,000/=	Ada ya Bweni	130,000/=
3.	Huduma ya chakula	300,000/=	Huduma ya chakula	300,000/=
4.	Matibabu	40,000/=	Matibatu	40,000/=
5.	Mitihani ya shule na taarifa kwa wazazi	30,000/=	Mitihani ya shule na taarifa kwa wazazi	30,000/=
6.	**JUMLA**	**850,000/=**	**JUMLA**	**850,000/=**

4.1 **UTARATIBU WA KULIPA**:

4.1.1 Lazima ulipe Tshs. 240,000/= za sare (wavulana) na Tshs. 210,000/= za sare (wasichana) siku ya kuja shuleni.

4.1.2 Unaweza ukalipa Tshs. 850,000/= nusu ya ada ya masomo na Hosteli muhula wa kwanza. Muhula wa pili ukalipa tena Tshs. 850,000/=

4.1.3 Unaweza ukalipa ada ya masomo na Hosteli mara nne kwa mwaka kwa utaratibu huu.

(a) Mwezi Julai -2018 Tshs. 425,000/=
(b) Mwezi Septemba- 2018 Tshs. 425,000/=
(c) Mwezi Januari 2018 Tshs. 425,000/=
(d) Mwezi April - 2018 Tshs. 425,000/=

MUHIMU: Shule haitapokea mwanafunzi asiyelipa ada kama tunavyoagiza. Kama huna Ada ya shule usije shuleni. Ukija bila ada utakurudisha nyumbani.

5. **FEDHA YA UCHAKAVU NA KITAMBULISHO:**

Kila mwanafunzi anatakiwa kulipa Tshs. 40,000/= ikiwa ni fedha ya kununulia vifaa vinapochakaa pamoja na Kitambulisho. Kila mwanafunzi aje na picha ndogo "stamp size" kwa ajili ya kitambulisho chake cha shule.

6. **UTARATIBU WA KULIPA FEDHA ZA SHULE:**

Fedha zote za shule hupelekwa Benki na mwanafunzi mwenyewe au mzazi wake. Hati za kulipia fedha hizi Benki zinatolewa shuleni. Fika ofisi namba 02 na 03 kwa Mhasibu wa Shule ili upate maelekezo ya kupeleka fedha Benki.

7. **RISITI ZA BENKI:**

Utakapomaliza kulipa fedha za shule kule Benki, unatakiwa ulete risiti za Benki shuleni siku hiyo hiyo. Usikae na risiti za Benki. Ukikaa nayo zaidi ya siku hiyo, tutakutoza faini ya Tshs. 6,000/= ndipo tupokee risiti yako. Hatutaki uzembe. Risiti hizi zipelekwe Ofisi namba 02 na 03 kwa Mtunza Fedha. Mr. Mahimbo. Usimpe mtu mwingine.

8. DAFTARI ZA SHULE

Kila mwanafunzi atanunua madaftari ya aina ya (COUNTER BOOKS" kwa ajili ya masomo anayosoma. Hatutaruhusu mwanafunzi kuja na datari za shule ya msingi. Masomo tunayofundisha kidato cha 5 ni haya:

(a) HKL - (Paper I, Paper II) na GS = Daftari 07
(b) HGL - (Paper I, Paper II) na GS = Daftari 07
(c) HGK - (Paper I, Paper II) na GS = Daftari 07
(d) CBG - (Paper I, Paper II) GS na B.A.M = Daftari 08
(e) PCB - (Paper I, Paper II) na GS = Daftari 08
(f) PCM - (Paper I, Paper II) na GS = Daftari 08

Daftari hizi lazima ziwe ni "COUNTER BOOKS" za mistari.

9. **MAHITAJI MAALUMU YA MASOMO YA SAYANSI:**

Wanafunzi wote wanaosoma masomo ya Sayansi yafuatayo lazima waje na vitabu au vifaa vifuatavyo:-

(a) CHEMISTRY:

Uje na kitabu kifuatacho. Nunua bookshop yoyote popote pale. CHEMSITRY FOR 'A' LEVEL & 1ST YEAR UNDERGRADUATE STUDENTS VOLUME I, PHYSICAL CHEMISTRY (MBP) by Ddungu, M. Schiess and others. Kitabu hiki ni mali yako ukimaliza shule utaenda nacho.

(b) **BIOLOGY:**

(i) Nunua kitabu hiki na uje nacho BIOLOGICAL SCIENCE 3rd EDITION by D. J. Taylor kitabu hiki ni mali yako, ukimaliza shule utaenda nacho.

(ii) **DISSECTING KIT**

Nunua DISSECTING KIT na uje nayo. KIT hii ni mali yako. Ukimaliza shule utaenda nayo.

(c) **GEOGRAPHY**:

Uje na kitabu hiki: PRINCIPALS OF PHYSICAL GEOGRAPHY by MONKHOUSE. Kitabu hiki ni mali yako. Ukimaliza shule utaenda nacho.

(a) **BASIC APPLIED MATHEMATICS**

Nunua kitabu hiki na uje nacho kwa ajili ya kusomea HISABATI. ADVANCED MATHEMATICS by SHAYO.

(b) **PHYSICS**
Uje na kitabu hiki "Advanced Physics" BY Nelkon M. 7th Edition. Hiki ni kitabu chako na si cha shule.

(c) **ADVANCED MATHEMATICS**
Uje na kitabu hiki PURE MATHEMATICS I na II by Backhouse J.K.

(d) wanafunzi wote wa masomo ya Sayansi lazima wanunue Scientific Calculators na waje nazo. Calculators hizi ni mali yao.

10. **VITU VINGINE AMBAVYO MWANAFUNZI WA HOSTELI ANAPASWA KUJA NAVYO:**

Vitu vituatavyo ununue na uje navyo shuleni:

1. Viatu vyeusi vya ngozi, vya kufunga ana Kamba, jozi au pea mbili. Viatu visiwe na kisigino kirefu, visivyochongoka, mbele viwe na sura ya ½ duara, uje na kiwi nyeusi ya kutosha.
2. Uje na Tshs. 3,000/= za picha za rangi
3. Daftari kubwa (Counter Books) za masomo yote ya combination yako.
4. "School Bag" moja nyeusi ya kubebea daftari na vitabu vyako.
5. Foronya moja ya pinki kwa wavulana na "Light Blue" kwa wasichana.
6. Kanga pea moja kwa wasichana.
7. Taulo moja rangi yoyote.
8. Sabuni za kufulia na kuogea za kutosha.
9. Mafuta ya kujipaka yasiyo na manukato.
10. Ndoo na Beseni la kufulia.
11. Nguo za michezo jozi mbili.
12. Raba za michezo na soksi jozi moja.
13. Kandambili za kuogea jozi moja.
14. Nguo za kulalia (night dress).
15. Sanduku la kuwekea mali yako na vitu vyote tulivyovitaja katika barua hii.
16. Kufuri imara la kufungia sanduku lako.
17. Miswaki miwili na dawa ya meno ya kutosha.
18. Fedha za matumizi yako binafsi (pocket money) kiasi kisichozidi 50,000/- kwa muhula.

11. **MASHARTI MAALUMU YA KUISHI HOSTELI:**

1. Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na kiasi cho chote cha Fedha Bwenini. Pesa yote ya matumizi ya mwanafunzi binafsi (Pocket money) itakabidhiwa kwa karai wa shule siku ya kufika shuleni.
2. Mwanafunzi haruhusiwi kupika chakula bwenini au kuleta au kuingiza chakula cha aina yo yote Bwenini kama vile Maziwa, Soda, Biskuti, Wali, Nyama, Chai, Sukari.
3. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa nguo za nyumbani. Nguo atakazovaa mwanafunzi ni zile sare za Hosteli tulizozitaja katika barua hii na si nguo zingine zozote.
4. Mwanafunzi hauruhusiwi kupunguza nguo au kubadilisha vipimo vya sare zake au kubadilisha suruali yake na kuwa VIMODO au kusilimu shati au T-Shirt yake.
5. Wanafunzi hawaruhusiwi kuingiza wageni hostelini au wanafunzi wa kutwa (day boys or day girls). Wageni wote waishie Ofisi ya Makamu wa Mkuu wa Shule (Second Master).
6. Wanafunzi wote lazima wafuate ratiba za kila siku za hosteli (daily routine).
7. Kila wakati wanafunzi wanapoenda likizo au wanapotoka likizo au wanapotoka nje ya mipaka ya shule, lazima wavae sare ya shule T-shirt nyekundu, suruali nyeusi au sketi nyeusi na viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba ya viatu.

8. **VITU VITUATAVYO USIJE NAVYO:**

   (a) Simu za mkononi
   (b) Radio
   (c) Silaha ya aina yoyote
   (d) Pasi ya mkaa au ya umeme. Shule itatoa pasi za umeme na za mkaa.
   (e) Kamera
   (f) Albamu za picha
   (g) Magazeti ya hadithi mfano SANI, UHONDO na mengine ya aina hii huruhusiwi kuja nayo shuleni.

9. Wanafunzi wakorofi, wagomvi, wasiofuata sheria za shule, na kanuni za hosteli watafukuzwa Hostelini mara moja na hatutarudisha fedha ulizolipa Hostelini.

10. Wanafunzi wote hawaruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila idhini ya Hosteli Meneja (Mwl. Nzala). Wanafunzi wanaotaka kwenda nyumbani wataomba ruhusa kwa Mkuu wa Shule. Watatakiwa kuandika barua ya kuomba ruhusa na Mkuu wa Shule atatoa ruhusa kwa Barua na nakala atapewa Hosteli Meneja.

11. Wanafunzi wote wanaoenda Kanisani au Msikitini lazima wavae sare ya shule. T-shirt, Suruali, Sketi au Hijabu na Viatu Vyeusi.

12. **MITIHANI YA KUINGIA KIDATO CHA 6:**

Kwa kuwa wanafunzi wengi wanaojiunga na shule yetu wanatoka shule mbalimbali za Kata na kwa kuwa wanafunzi wengi wanaoomba kuingia Kidato cha 5 hapa kwetu ni wale ambao hawajachaguliwa kujiunga na Shule za Sekondari za Serikali na kwa kuwa wanafunzi wamekaa nyumbani zaidi ya miezi mitatu na hivyo kukaa bila kujisomea kwa muda mrefu, Shule haitatoa mitihani ya kujiunga na masomo ya kidato cha 5. Wanafunzi wote watalipia fomu za kujiunga na shule na kuanza masomo yao ya kidato cha tano mara moja kuanzia mwezi Julai hadi mwezi Mei ya mwaka unaofuata. Mwezi Mei ya mwaka unaofuata wanafunzi wote watafanya mtihani wa kumaliza kidato cha 5. Wanafunzi watakaofaulu mtihani huo na kupata wastani wa asilimia 50 (50%) wataingia kidato cha 6 wakiwa watahiniwa wa Shule (School Candidates) na wale watakaokosa kupata wastani huo watafanya mtihani wao kama watahiniwa wa kujitegemea (Private Candidates). Wanafunzi wote wanaagizwa kusoma kwa bidii ili kuweza kufikia malengo yetu ya shule kwa faida yao. Wanafunzi wote watakaoingia kidato cha 6 lazima wafaulu na majina yao kupitishwa na Bodi ya shule.

13. **SHERIA ZA SHULE:**

Wanafunzi wote watakapofika shuleni watasomewa Sheria za Shule. Wanafunzi wote watakaopatikana na makosa yoyote ya kinidhamu, watapata adhabu zifuatazo:-

(a) Kufanya kazi ngumu
(b) Kuchapwa viboko
(c) Kusimamishwa shule
(d) Kufukuzwa shule

14. **USAFI:**

(a) Kila mwanafunzi anatakiwa awe nadhifu (msafi) daima.
(b) Kila mwanafunzi atafagia darasa lake kwa zamu
(c) Kila mwanafunzi atadeki darasa lake kila Ijumaa jioni saa 11 - 12½ kwa zamu.
(d) Kila mwanafunzi atafagia eneo la shule kwa zamu
(e) Kila darasa litakuwa na watu maalum wa kufyeka eneo la darasa lao kama itakavyopangwa na Kiranja Mkuu.

15. **MONTHLY TESTS:**

Wanafunzi wote watatakiwa kufanya mitihani yao ya kila mwezi. Watakaoacha kufanya "Monthly Tests" zao watasimamishwa shule na au kufukuzwa shule. Wanafunzi wote lazima wafaulu mitihani yao na wapate wastani wa kuanzia asilimia 50 (50%) na kuendelea.

16. **BEGI LA SHULE (SCHOOL BAG)**

Kila mwanafunzi anaagizwa kununua begi zuri la kutunzia daftari na vitabu vyake. Wanafunzi hawaruhusiwi kuja shuleni huku wamebeba daftari zao na vitabu vyao mikononi.

17. **KARATASI ZA KUJIBU MITIHANI (RIMU)**

Kila mwanafunzi anaagizwa kuleta Bunda (ream) moja ya karatasi za mistari (Ruled paper) za kujibia mitihani yake. Karatasi hizi zipelekwe kwa Mwalimu Mwandamizi Taaluma (Senior Academic Master) Chumba na 06.

18. **LUGHA YA SHULE:**

Lugha ya shule ni Kiingereza. Wanafunzi wote wanatakiwa kuzungumza Kiingereza tu muda wote wanapokuwa shuleni. Hii ni sheria ya shule na ni sheria ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Sheria hii inaitwa "THE SPEAK ENGLISH RULE." Wanafunzi wote wanaagizwa kuongea Kiingereza na walimu wao na wanafunzi wenzao. Wanafunzi watakaozungumza Kiswahili shuleni watapewa adhabu ya kufanya kazi ngumu.

19. **KUTUNZA MAZINGIRA YA SHULE:**

Wanafunzi wote wanatakiwa kutunza mazingira ya shule vizuri. Wanafunzi wote wanaagizwa kuacha tabia za kutupa karatasi ovyo, kutupa mifuko ya karanga ovyo baada ya kula karanga, kutupa ovyo mifuko ya plastic ya Barafu. Wanafunzi wote watembee katika barabara zilizopo shuleni wasitumie njia za mkato au njia za panya. Wanafunzi wote kwa zamu, watatakiwa kufyeka maeneo ya shule, kureki majani baada ya kufyeka, kupanda maua, miti ya kiuvuli na miti ya matunda. Wanafunzi wote wanatakiwa kumwagilia miti na maua watakayoagizwa kupanda. Kumbuka kuweka mazingira ya shule yako safi ni wajibu wa kila mwanafunzi.

20. **UPIMAJI WA AFYA ZA WANAFUNZI:**

Wanafunzi wote wanaojiunga na shule wanatakiwa kupima afya zao kabla ya masomo kuanza rasmi. Kila mwanafunzi atapewa Fomu ya kupimia afya yake. Fomu hizi zijazwe na Daktari wa Hospitali hiyo ambayo mwanafunzi alipima Afya yake. Zoezi la kupima Afya ni endelevu. Shule inawataka wanafunzi wote kupima afya zao kila muhula wanapotoka likizo. Kila mzazi atalipia gharama zote za upimaji wa Afya ya mwanae kila mara shule inapofunguliwa.

21. **KUJIPANGA PARADI:**

Kila mwanafunzi anaagizwa kuwahi kuja shuleni kila siku. Wanafunzi wote wanatakiwa kufika shuleni saa moja asubuhi ili kufagia maeneo yao. Saa 1½ asubuhi wanafunzi wote lazima wajipange kwenye uwanja wa Parade. Hapo wanafunzi wote wataimba wimbo wa Taifa siku ya Jumatatu na Alhamisi tu. Wimbo wa Taifa unatakiwa kuheshimiwa sana na siyo wimbo wa kuimbwa ovyo ovyo. Siku za Jumanne, Jumatano na Ijumaa, wanafunzi wote wataimba wimbo wa TANZANIA, TANZANIA NAKUPENDA KWA MOYO WOTE. Wimbo wa Taifa na wimbo wa Tanzania Nakupenda zinaweza kuimbwa pamoja kwa maagizo maalumu kutoka kwa mwalimu wa zamu, Second Master au Mkuu wa shule ama pale panapokuwa na wageni shuleni. Wanafunzi wote wanaagizwa kujipanga kwenye uwanja wa Paredi. Kuacha kufika kwenye Parade ni kosa, wanafunzi wasiofika kwenye Parade wataadhibiwa vikali sana.

22. **AKAUNTI ZA SHULE:**

Fedha zote za shule ziwekwe kwenye Akaunti za shule kama ifuatayo:

(a)	Ada ya shule na Fedha ya tahadhari	**A/C – 024101001942 NBC LTD**
(B)	Fedha ya Sare	**A/C - 024101001030 NBC LTD**
(c)	Fedha ya Usajiri	**A/C – 024101001917 NBC LTD**

Huruhusiwi kuja na hela ya malipo yoyote shuleni.

JOHN .A. NDAMA
KAIMU MKUU WA SHULE

SHINYANGA REGION CO-OPERATIVE UNION (1984) LTD.
BULUBA SECONDARY SCHOOL

S.L.P. 173, SHINYANGA Tel. No 028 – 2763380 Mob.0764-478683/0683501913
Email: bulubass@yahoo.com

Tarehe 02 FEBRUARY, 2018

Jina la Mwanafunzi: …….
Kidato cha TANO

YAH: **MAAGIZO MUHIMU KWA WANAFUNZI WOTE WA KUTWA WANAOINGIA KIDATO CHA TANO**

1. **TAREHE YA KUANZA MASOMO**:

Masomo yataanza rasmi tarehe 02 July mwaka 2018. Wanafunzi wote wanatakiwa kufika shuleni saa 1 na dakika 30 asubuhi.

2. **NGUO ZA KUANZIA MASOMO:**

Kabla ya kupata sare rasmi za Shule, wanafunzi wote wavae sare za Shule za Sekondari walikomalizia kidato cha 4 mwaka jana. Wanafunzi wote watavaa viatu vyeusi vya ngozi, ambavyo vitakuwa nusu mviringo kwa upande wa mbele. Viatu vya mstatiri (square) havitakiwi. Visigino vya viatu visiwe virefu (Raizoni). Wasichana watavaa soksi fupi nyeupe.

3. **SARE RASMI ZA SHULE:**

Sare rasmi za shule zinauzwa shuleni. Sare za shule zifuatazo zitanunuliwa hapa hap shuleni. Ili kupata sare mwanafunzi awasiliane na Makamu Mkuu wa Shule Mwalimu Makoye Nzala.

(a) **KWA WASICHANA:**

NA.	SARE	BEI YAKE
1.	Sketi mbili nyeusi na kikoti chake cheusi	Tshs. 30,000/=
2.	Shati mbili nyeupe mikono mirefu za kuvaa asubuhi	Tshs. 25,000/=
3.	T-shirt mpya ya shule ya rangi nyekundu ya kuvaa jioni	Tshs. 10,000/=
4.	Sweta la shule rangi ya Bluu la kuvaa wakati wa baridi	Tshs. 15,000/=
JUMLA KUU		**Tshs. 80,000/=**

(b) **HIJABU:**
Wanafunzi wanaotaka kuvaa hijabu watalipa Tshs. 90,000/= ikiwa ni gharama ya kununua Hijabu ya Asubhi na Jioni, Sweta na Sruali mbili nyeusi.

(c) **KWA WAVULANA:**

NA.	SARE	BEI YAKE
1.	Shati mbili nyeupe za mikono mirefu za kuvaa asubuhi	Tshs. 25,000/=
2.	T-shirt nyekundu ya shule ya kuvaa jioni	Tshs. 10,000/=
3.	Suruali mbili nyeusi	Tshs. 36,000/=
4.	Tai mpya ya shule ya kuvaa asubuhi	Tshs. 5,000/=
5.	Sweta la shule la rangi ya Bluu la kuvaa wakati wa baridi	Tshs. 15,000/=
6.	Mkanda wa shule wa kuvalia suruali	Tshs. 6,000/=
JUMLA KUU		**Tshs. 97,000/=**

Sare zote za shule zitanunuliwa shuleni. Usinunue sare za shule nje ya shule yetu. Huu ndiyo utaratibu wetu. Fedha za sare zilipwe kwenye akaunti ya Shule ya Sare.

4. **ADA YA SHULE:**

Ada ya Shule kwa mwaka ni Tshs. 900,000/= tu. Ada hii inalipwa mara mbili kwa mwaka.

(a) Mwezi JULAI – Lipa Tshs. 450,000/= tu
(b) Mwezi JANUARI – Lipata Tshs. 450,000/= tu

MUHIMU: Shule haitapokea mwanafunzi asiyelipa ada kama tunavyoagiza. Kama huna Ada ya shule usije shuleni. Ukija bila ada utakurudisha nyumbani.

5. **FEDHA YA UCHAKAVU:**

Kila mwanafunzi anatakiwa kulipa Tshs. 40,000/= ikiwa ni fedha ya kununulia vifaa vinapochakaa pamoja na Kitambulisho. Kila mwanafunzi aje na picha ndogo "stamp size" kwa ajili ya kitambulisho chake cha shule.

6. **UTARATIBU WA KULIPA FEDHA ZA SHULE:**

Fedha zote za shule hupelekwa Benki na mwanafunzi mwenyewe au mzazi wake.

7. **RISITI ZA BENKI:**

Utakapomaliza kulipa fedha za shule kule Benki, unatakiwa ulete risiti za Benki shuleni siku hiyo hiyo. Usikae na risiti za Benki. Ukikaa nayo zaidi ya siku hiyo, tutakutoza faini ya Tshs. 6,000/= ndipo tupokee risiti yako. Hatutaki uzembe. Risiti hizi zipelekwe Ofisi namba 02 na 03 kwa Mtunza Fedha. Mr. Mahimbo. Usimpe mtu mwingine.

8. DAFTARI ZA SHULE

Kila mwanafunzi atanunua madaftari ya aina ya (COUNTER BOOKS" kwa ajili ya masomo anayosoma. Hatutaruhusu mwanafunzi kuja na datari za shule ya msingi. Masomo tunayofundisha kidato cha 5 ni haya:

(a) HKL - (Paper I, Paper II) na GS = Daftari 07
(b) HGL - (Paper I, Paper II) na GS = Daftari 07
(c) HGK - (Paper I, Paper II) na GS = Daftari 07
(d) CBG - (Paper I, Paper II) GS na B.A.M = Daftari 08
(e) PCB - (Paper I, Paper II) na GS = Daftari 08
(f) PCM - (Paper I, Paper II) na GS = Daftari 08
(g) EGM - (Paper I, Paper II) GS na B.A.M = Daftari 08

Daftari hizi lazima ziwe ni "COUNTER BOOKS" za mistari.

9. **MAHITAJI MAALUMU YA MASOMO YA SAYANSI:**

Wanafunzi wote wanaosoma masomo ya Sayansi yafuatayo lazima waje na vitabu au vifaa vifuatavyo:-

(b) CHEMISTRY:

Uje na kitabu kifuatacho. Nunua bookshop yoyote popote pale. CHEMSITRY FOR 'A' LEVEL & 1ST YEAR UNDERGRADUATE STUDENTS VOLUME I, PHYSICAL CHEMISTRY (MBP) by Ddungu, M. Schiess and others. Kitabu hiki ni mali yako ukimaliza shule utaenda nacho.

(b) **BIOLOGY:**

(i) Nunua kitabu hiki na uje nacho BIOLOGICAL SCIENCE 3rd EDITION by D. J. Taylor kitabu hiki ni mali yako, ukimaliza shule utaenda nacho.

(ii) **DISSECTING KIT**

Nunua DISSECTING KIT na uje nayo. KIT hii ni mali yako. Ukimaliza shule utaenda nayo.

(c) **GEOGRAPHY**:

Uje na kitabu hiki: PRINCIPALS OF PHYSICAL GEOGRAPHY by MONKHOUSE. Kitabu hiki ni mali yako. Ukimaliza shule utaenda nacho.

(a) **BASIC APPLIED MATHEMATICS**

Nunua kitabu hiki na uje nacho kwa ajili ya kusomea HISABATI. ADVANCED MATHEMATICS by SHAYO.

(b) **PHYSICS**

Uje na kitabu hiki "Advanced Physics" BY Nelkon M. 7th Edition. Hiki ni kitabu chako na si cha shule.

(c) **ADVANCED MATHEMATICS**

Uje na kitabu hiki PURE MATHEMATICS I na II by Backhouse J.K.

(d) wanafunzi wote wa masomo ya Sayansi lazima wanunue Scientific Calculators na waje nazo. Calculators hizi ni mali yao.

10. **MITIHANI YA KUINGIA KIDATO CHA 6:**

Kwa kuwa wanafunzi wengi wanaojiunga na shule yetu wanatoka shule mbalimbali za Kata na kwa kuwa wanafunzi wengi wanaoomba kuingia Kidato cha 5 hapa kwetu ni wale ambao hawajachaguliwa kujiunga na Shule za Sekondari za Serikali na kwa kuwa wanafunzi wamekaa nyumbani zaidi ya miezi mitatu na hivyo kukaa bila kujisomea kwa muda mrefu, Shule haitatoa mitihani ya kujiunga na masomo ya kidato cha 5. Wanafunzi wote watalipia fomu za kujiunga na shule na kuanza masomo yao ya kidato cha tano mara moja kuanzia mwezi Julai hadi mwezi Mei ya mwaka unaofuata. Mwezi Mei ya mwaka unaofuata wanafunzi wote watafanya mtihani wa kumaliza kidato cha 5. Wanafunzi watakaofaulu mtihani huo na kupata wastani wa asilimia 50 (50%) wataingia kidato cha 6 wakiwa watahiniwa wa Shule (School Candidates) na wale watakaokosa kupata wastani huo watafanya mtihani wao kama watahiniwa wa kujitegemea (Private Candidates). Wanafunzi wote wanaagizwa kusoma kwa bidii ili kuweza kufikia malengo yetu ya shule kwa faida yao. Wanafunzi wote watakaoingia kidato cha 6 lazima wafaulu na majina yao kupitishwa na Bodi ya shule.

11. **SHERIA ZA SHULE:**

Wanafunzi wote watakapofika shuleni watasomewa Sheria za Shule. Wanafunzi wote watakaopatikana na makosa yoyote ya kinidhamu, watapata adhabu zifuatazo:-

(e) Kufanya kazi ngumu
(f) Kuchapwa viboko
(g) Kusimamishwa shule
(h) Kufukuzwa shule

12. **USAFI:**

(f) Kila mwanafunzi anatakiwa awe nadhifu (msafi) daima.
(g) Kila mwanafunzi atafagia darasa lake kwa zamu
(h) Kila mwanafunzi atadeki darasa lake kila Ijumaa jioni saa 11 - 12½ kwa zamu.
(i) Kila mwanafunzi atafagia eneo la shule kwa zamu
(j) Kila darasa litakuwa na watu maalum wa kufyeka eneo la darasa lao kama itakavyopangwa na Kiranja Mkuu.

13. **MONTHLY TESTS:**

Wanafunzi wote watatakiwa kufanya mitihani yao ya kila mwezi. Watakaoacha kufanya "Monthly Tests" zao watasimamishwa shule na au kufukuzwa shule. Wanafunzi wote lazima wafaulu mitihani yao na wapate wastani wa kuanzia asilimia 50 (50%) na kuendelea.

14. **VITU VISIVYORUHUSIWA:**

Wanafunzi wote hawaruhusiwi kuja na vitu vifuatavyo shuleni:

(a) Kamera
(b) Radio
(c) Simu za mkononi
(d) Silaha
(e) Albamu za picha
(f) Magazeti ya Hadithi mfano SANI, UHONDO na mengine ya aina hii huruhusiwi kuja nayo shuleni

Mwanafunzi atakayekamatwa akiwa na vitu hivi shuleni au kimoja ya vitu hivyo atafukuzwa shule mara moja.

15. **BEGI LA SHULE (SCHOOL BAG)**

Kila mwanafunzi anaagizwa kununua begi zuri la kutunzia daftari na vitabu vyake. Wanafunzi hawaruhusiwi kuja shuleni huku wamebeba daftari zao na vitabu vyao mikononi.

16. **KARATASI ZA KUJIBU MITIHANI (RIMU)**

Kila mwanafunzi anaagizwa kuleta Bunda (ream) moja ya karatasi za mistari (Ruled paper) za kujibia mitihani yake. Karatasi hizi zipelekwe kwa Mwalimu Mwandamizi Taaluma (Senior Academic Master) Chumba na 06.

17. **BAISKELI SHULENI:**

Shule haiagizi mwanafunzi kuja na baiskeli shuleni. Lakini wanafunzi wanakuja na baiskeli shuleni kwa hiari yao. Wanafunzi watakaokuja na baiskeli wahakikishe kuwa baiskeli zao zina kufuri na zinafungwa. Wanafunzi hawahurusiwi kuazima baiskeli zao kwa mtu yo yote hata kama ni mwalimu wa shule hii. Mwanafunzi yeyote atakayepoteza baiskeli yake shule haitahusika, ila anaagizwa kwenda kituo cha Polisi na Polisi watamsaidia kupata baiskeli yake.

18. **LUGHA YA SHULE:**

Lugha ya shule ni Kiingereza. Wanafunzi wote wanatakiwa kuzungumza Kiingereza tu muda wote wanapokuwa shuleni. Hii ni sheria ya shule na ni sheria ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Sheria hii inaitwa "THE SPEAK ENGLISH RULE." Wanafunzi wote wanaagizwa kuongea Kiingereza na walimu wao na wanafunzi wenzao. Wanafunzi watakaozungumza Kiswahili shuleni watapewa adhabu ya kufanya kazi ngumu.

19. **KUTUNZA MAZINGIRA YA SHULE:**

Wanafunzi wote wanatakiwa kutunza mazingira ya shule vizuri. Wanafunzi wote wanaagizwa kuacha tabia za kutupa karatasi ovyo, kutupa mifuko ya karanga ovyo baada ya kula karanga, kutupa ovyo mifuko ya plastic ya Barafu. Wanafunzi wote watembee katika barabara zilizopo shuleni wasitumie njia za mkato au njia za panya. Wanafunzi wote kwa zamu, watatakiwa kufyeka maeneo ya shule, kureki majani baada ya kufyeka, kupanda maua, miti ya kiuvuli na miti ya matunda. Wanafunzi wote wanatakiwa kumwagilia miti na maua watakayoagizwa kupanda. Kumbuka kuweka mazingira ya shule yako safi ni wajibu wa kila mwanafunzi.

20. **UPIMAJI WA AFYA ZA WANAFUNZI:**

Wanafunzi wote wanaojiunga na shule wanatakiwa kupima afya zao kabla ya masomo kuanza rasmi. Kila mwanafunzi atapewa Fomu ya kupimia afya yake. Fomu hizi zijazwe na Daktari wa Hospitali hiyo ambayo mwanafunzi alipima Afya yake. Zoezi la kupima Afya ni endelevu. Shule inawataka wanafunzi wote kupima afya zao kila muhula wanapotoka likizo. Kila mzazi atalipia gharama zote za upimaji wa Afya ya mwanae kila mara shule inapofunguliwa.

21. **KUJIPANGA PAREDI:**

Kila mwanafunzi anaagizwa kuwahi kuja shuleni kila siku. Wanafunzi wote wanatakiwa kufika shuleni saa moja asubuhi ili kufagia maeneo yao. Saa 1½ asubuhi wanafunzi wote lazima wajipange kwenye uwanja wa Parade. Hapo wanafunzi wote wataimba wimbo wa Taifa siku ya Jumatatu na Alhamisi tu. Wimbo wa Taifa unatakiwa kuheshimiwa sana na siyo wimbo wa kuimbwa ovyo ovyo. Siku za Jumanne, Jumatano na Ijumaa, wanafunzi wote wataimba wimbo wa TANZANIA, TANZANIA NAKUPENDA KWA MOYO WOTE. Wimbo wa Taifa na wimbo wa Tanzania Nakupenda zinaweza kuimbwa pamoja kwa maagizo maalumu kutoka kwa mwalimu wa zamu, Second Master au Mkuu wa shule ama pale panapokuwa na wageni shuleni. Wanafunzi wote wanaagizwa kujipanga kwenye uwanja wa Paredi. Kuacha kufika kwenye Parade ni kosa, wanafunzi wasiofika kwenye Parade wataadhibiwa vikali sana.

22. **AKAUNTI ZA SHULE:**

Fedha zote za shule ziwekwee kwenye Akaunti za shule kama ifuatavyo:-

(a) Ada ya Shule na fedha ya tahadhari **A/C – 024101001942 NBC LTD**
(b) Fedha ya Sare **A/C - 024101001030 NBC LTD**
(c) FEdha ya Usajili **A/C - 024101001917 NBC LTD**

Huruhusiwi kuja na hela ya malipo yoyote shuleni.

JOHN .A. NDAMA
KAIMU MKUU WA SHULE